


# MUDA KWA HARAKA SANA UNAKWISHA!

USHUHUDA WA VICTORIA NEHALE – NCHINI NAMIBIA

# UTANGULIZI

Nimezaliwa na kuishi Namibia maisha yangu yote. Niliokoka tarehe 06/02/2005. Bwana Yesu amenifunulia mambo mengi ya ulimwengu wa roho pamoja na kunipeleka mara kadhaa kuzimu.
Bwana aliniambia niwaelezee watu niliyoyaona; na akanionya nisiongeze wala kupunguza chochote kwa yale aliyonionyesha au kuniambia. Kufikia kuandika kitabu hiki, mwisho wa 2006, nilikuwa nimetembelewa na Bwana Yesu mara 33. Kwa kila utembezi huo Bwana alinisisitizia: **MUDA UMEISHA**.

## SAFARI YA KWANZA KWENDA KUZIMU

Mwisho wa juma la 23/07/2005, nilichukua teksi kutoka mji wa Ondangwa (Nchini Namibia) ninakoishi na kufanya kazi, kuelekea kijijini kwetu kuwaona wazazi wangu. Nilipokwa njiani nilihisi kuwa kitu cha ajabu kilikuwa kinaenda kutokea jioni hiyo. Nilifika nyumbani mwendo wa saa kumi na mbili jioni na ndio wakati watu walikuwa wakiandaa chakula cha jioni. Nilikuwa jikoni na ndugu zangu nimelala juu ya shuka kukuu chini, na wapwa zangu walikuwa wakiimba nyimbo za kanisani.

Ghafla nikahisi nguvu kuu za Mungu juu yangu zilizoufanya mwili wangu kuzimia. Nilimwona mtu mwenye kanzu nyeupe na kamba yenye rangi sawa, akinisogelea nilipokuwa nimelala. Kulikuwa na mwanga wa ajabu unamzunguka kana kwamba unatoka kwake. Alikuwa amevaa viatu vya hudhurungi. Alifanana na watu wa mashariki ya kati hata ngozi ikawa inampendeza. Mwili wake ulikuwa umejaa utukufu nilishindwa kumwangalia kwenye macho. Alipoongea sauti yake ilikuwa ya upole, huruma, upendo, na yenye mamlaka. Mawimbi ya upendo yalikuwa yakinijia kutoka kwake.

Akainyosha mikono yake kuelekea kwangu na kuniinua. Ghafla nikajikuta nipo katika mwili mzuri uliobadilishwa. Nilionekana kama vile nilivyo kuwa kijana wa miaka kumi na nane. nilikuwa nimevalia kanzu nyeupe iliyofungwa kamba nyeupe. Ijapokuwa kanzu yangu ilikuwa nyeupe lakini malighafi yake ilikuwa tofauti na kanzu yake. Vazi lake lilikuwa la kitani safi na mwanga na mng'ao wake ni vigumu kuelezea.

Alisema kwa upendo na sauti ya upole, ***''Victoria fuatana nami, nitakuonyesha mambo ya kuogopesha na kukupeleka sehemu ambayo hujawahi kuona maisha yako yote***".
Akanishika mkono wa kuume na tukaanza kuenda. Nilihisi kama vile tunatembea hewani na tunapanda wakati wote. Baada ya muda njiani nikawa nimechoka sana. Nikamwambia nisingeweza kuendelea na safari na nikaomba kurudi nyumbani.

Aliniangalia kwa upole na kusema "***Haujachoka uko safi, ukichoka nitakubeba. Lakini sasa uko safi. Amani na iwe nawe, tuondoke***".
Sehemu tuliyofika ilikuwa kame na mbaya kuliko jangwa lolote baya lililojulikana na binadamu, bila dalili yoyote ya uhai au maisha. Hapakuwa na mti wowote, nyasi au kiumbe chenye uhai hakikuonekana. Ilikuwa ni sehemu mbaya sana.
Tulikuja kwenye lango na yule mtu akanigeukia akisema, "***Victoria tutapitia langoni na vitu utakavyofundishwa vitakuogopesha na kukufadhaisha. Lakini uwe na uhakika kokote nitakako kupeleka utalindwa vizuri. Fungua macho yako uangalie kila kitu nitakacho kuonyesha***".
Nilitishika na kuanza kulia. Nilipinga na kutaka anirudishe.
Nikamwambia kuwa sikutaka kuingia mahali pale kwakuwa nilikuwa naona yanayotendeka ndani akaniambia, ***"Amani na iwe nawe; niko pamoja nawe ni lazima tuingie ndani, kwa maana MUDA UMEISHA".***

## Kuzimu kulivyo

Tukapita lango lile mpaka ndani na kwa niliyoyaona nashindwa kusimulia mahali pale palivyo. Nina uhakika hakuna mahali pengine duniani pa kutisha kama pale. Mahali pale palikuwa pakubwa sana na nilihisi kuwa palikuwa panaongezeka wakati wote. Giza la mahali pale lilikuwa kubwa sana na moto uliokuwa unawaka haupimiki. Moto wenyewe au miali yake ilikuwa

haionekani ila ukali wake ulikuwa juu sana. Nzi wa kila namna na rangi walikuwa kila mahali. Palikuwepo pia na minyoo wafupi, wanene na weusi wakijaribu kupanda juu ya kila kitu. Minyoo wakanza kupanda juu yetu huku inzi wakiruka kila mahali. Harufu ya mahali pale ilikuwa mbaya mno, ilikuwa kama  nyama iliyooza ila ni zaidi ya mara mia ya harufu yoyote ile niliyo wahikuihisi. Kulikuwa kumejaa sautu za vilio na kusaga meno, pia nilisikia vicheko viovu vya pepo wabaya.

Cha kuhuzunisha ni kuwa mahali pale palikuwa pamejaa watu wasiohesabika.  Watu walikuwa kwa namna ya mifupa. Nilijua mifupa hiyo ilikuwa ni watu kwani niliweza kwa uhakika kuwajua ndugu zangu kutoka kijijini kwetu. Mifupa hiyo ya rangi ya kijivu ilikuwa imekauka sana. Walikuwa na meno makali  kama ya wanyama,  midomo mikubwa na ndimi ndefu na nyekundu. Mikono na miguu ilikuwa na vidole virefu vyenye kucha za kutisha. Wengine walikuwa na mikia na pembe.

Pepo wachafu walikuwa wakichangamana na watu. Mapepo hao walikuwa kama kenge wakitembea kwa miguu minne. Waliifurahia hali ile na wakawa wakiwatesa na kuwakejeli wanadamu, huku wao wakirukaruka na kushangilia wakati wote. Wanadamu kwa upande wao walionekana wa kusikitisha na kuvunjika moyo, walionekana kukata tamaa na bila matumaini yoyote. Kelele za wanadamu zilikuwa kwasababu ya maumivu. Walikuwa wakilia, kupaza sauti na kusaga meno. Hali yao haikuwa ya kusikitisha tu, bali pia ya uchungu na masitikiko.Watu wa mahali pale walikuwa wengi lakini niliona wazi kuwa wengi walikuwa wanawake.

## Makundi ya watu kuzimu

Waligawanywa kwa makundi tofauti lakini haikuwezekana kuwahesabu kwa makundi yao kwani walikuwa wengi sana. Niliyekuwa naye akanipeleka kwa kikundi kimoja cha mashariki na kuniambia, “*Hili ni kundi la walioshindwa KUSAMEHE. Niliwaeleza mara nyingi na kwa njia tofauti jinsi ya kuwasamehe wenzao lakini wao wakakataa. Niliwasamehe dhambi zao zote lakini wao wakakataa kuwasamehe wengine. Muda wao duniani ulipoisha wakajipata mahali hapa. Watakuwa mahali milele yote, wanavuna matunda ya matendo yao milele na milele. Ila ni uchungu kwangu kuwaona hapa katika hali hii – kwa kuwa nawapenda”.*

Nikaongozwa kwa kundi la pili na nikaambiwa na yule mwenye kunipeleka, kuwa walikuwa wenye **MADENI** na makundi yao yalikuwa matatu:

1. Wa kwanza ni wale waliodaiwa na wenzao na walikuwa na uwezo wa kulipa lakini wakawa wakihairisha siku baada ya siku. Wangeahidi kulipa wakati ujao, mwezi ujao, mwaka ujao mpaka muda wao duniani ukaisha na wakajipata mahali hapa. Watakaa mahali hapa milele na milele wanavuna matunda ya kazi yao.

2. Wa pili ni wale waliodaiwa madeni waliyoweza kulipa na walikuwa tayari kulipa lakini waliogopa madhara yake. Waliona kuwa wakiongea ukweli watakataliwa, watapelekwa jela au walichokifanya kingejulikana dunia yote na wangedhalilishwa. Yule mtu akaniambia, “Hakuna hata mmoja aliyeniuliza njia ya kulipa. Wangefanya hivyo ningewaonyesha njia rahisi. Walitumia hekima na sababu zao ambazo hazikuwasaidia hata kidogo”.

3. Waliokuwa na madeni wasiyoweza kulipa ila hawakuniambia kwamba wana madeni wasiyoweza kulipa. Wangefanya hivyo ningewalipia madeni yao. Pia walijaribu kutumia hekima na sababu zao, ambazo hazikuwasaidia hata kidogo. Sasa wamejikuta sehemu hii wasiyoweza kutoka. Wanakula matunda ya matendo yao. Moyo waniuma kwa ajili ya hawa wote kwasababu nawapenda sana.

Katika kundi la kwanza niliwaona ndugu zangu wawili wa kike wa karibu, vilevile na ndugu yangu mmoja wa miaka kumi na miwili. Nilijua miaka yake kwani huo ndio uliokuwa umri wake alipofariki. Katika kundi la pili niliwaona baadhi ya ndugu zangu na hata mchungaji niliyekuwa namfahamu vizuri. Jakes mpenzi wangu aliyejinyonga baada ya mimi kuokoka  alikuwa kwenye kundi la pili. Niliwaona baadhi ya majirani  zangu katika makundi yote.

Niliwajua watu tuliokuwa tukifahaminiana na wao pia wakanijua. Watu wa ukoo wetu waliponiona walianza kunitukana kwa lugha chafu. Mmoja wao akaniambia kuwa sikustahili

kumfuata yule niliye kuwa naye. Wakanikumbusha hali niliyokuwa kabla ya wokovu. Waliyoyasema yalikuwa kweli kwani ni mambo niliyoyafanya. Jakes mpenzi wangu akasema kuwa nilikuwa wake na nilistahili kuwa alipokuwa maana dhambi zetu zilikuwa sawa. Mwanzoni Mchungaji alifurahia kuniona nikienda alikokuwa, lakini alipoona niliyeandamana naye akaungana na wenzie kunitukana. Aliyekuwa nami akaniambia niyapuuzie maneno hayo kwani hawakujua walichokuwa wakifanya.

Nikaogopa na kushikwa na huzuni sana, nilikuwa nikitetemeka nikashindwa kusimama. Nikalia bila kujizuia ndipo niliyekuwa naye akanikumbatia na kusema, "***Amani na iwe nawe Victoria***". Palepale nguvu zikanirudia na nikapata faraja na amani kuwa naye. Wakati wa kuondoka ukawa umefika naye akasema, "***Victoria nimekuonyesha haya ili uchague ni kundi lipi ungependa kuwa, kwa kuwa uamuzi ni wako. Lazima uwaambie watu kila kitu ulichoona bila kupunguza au kuongeza kitu chochote***."

## Kurudi kutoka kuzimu

Nakumbuka tulipotoka mahali pale pa mateso tukiwa pamoja, ila sijui nilipomuacha kwasababu niliposhtuka na kufungua macho nilijikuta mwilini kama kawaida. Nilikuwa nimelazwa hospitali ya Oshakati. Kulikuwa na mpira wa kuingizia maji mwilini, mamangu na ndugu zangu walikuwa chumbani humo. Machozi yalikuwa hayajamkauka mamangu. Nilipomuuliza Nesi kilichokuwa kikiendelea akaniambia, "Umerudishwa, pengine una makosa na unahitaji kutubu."
Japo Nesi aliongea kwa furaha bado niliona anaogopa kunisogelea. Nikamuulizia daktari aliyekuwa akinishughulikia.

Daktari alipofka hakuweza kuelezea ugonjwa niliokuwa nao. Alidhania kuwa malaria lakini matokeo hayakuonyesha hivyo. Joto la mwili na shinikizo la damu vyote vilikuwa chini sana lakini hakujua sababu yake. Hakujua la kufanya kwani hangeweza kunilaza Hospitalini kwani sikuwa mgonjwa. Maji waliyoniingizia kwa mpira yalikuwa hayaingii vizuri lakini mara tu nilipofungua macho yakaanza kuingia bila tatizo. Daktari akaagizia niongezewe maji mengine.

Niliendelea kuhofu na kulia kwa ajili ya mahali pale pa mateso. Matukio ya mahali pale yaliendelea kupita machoni kwangu saa zote. Sikuweza kulala mwili mzima ulikuwa unaumwa, viungo vyote vilikuwa kama vimetenganishwa na kuunganishwa tena. Tumbo lilinisumbua na kichwa kikaniuma juma zima.

Niliamua kutomwelezea mtu yeyote niliyoyaona. Ni nani atakayeniamini? Watu wangenichukuliaje? Nikajiwazia. Baada ya siku tatu nikamwambia mama mmoja aniombee na nikaishia kumwelezea yote yaliyotokea. Nikajihuzunikia sana kwa kuisimulia hadithi hiyo maana sasa haingeweza kufichika. Mwishowe nilielewa kuwa Mungu ni Mungu. Akitaka kitu kisimuliwe sina uwezo wa kukizuia eti kwasababu ya ya mawazo na hofu yangu.

## Maelezo juu ya safari

Agosti 19, niliamka nikihisi nguvu za Mungu. Nilikuwa dhaifu nikitetemeka na nikajisikia kama nguvu za umeme zinapita mwilini. Jioni nikaona miale ya mwanga mkuu na katikati yake nikamwona mtu yule aliyenipeleka sehemu ya mateso. Wakati huu akaketi kwenye kiti karibu na kitanda changu. Kiti chenyewe hakikuwepo lakini alipotaka kukaa kilionekana. Kilikuwa kiti cha mapambo mazuri huku kikiwa kimeundwa na dhahabu tupu.

Baada ya kunisalimia akaniambia kuwa anaelewa kuwa nina maswali mengi na ndio maana alikuwa amejitokeza ili ajieleze yeye na mambo mengine yaliyokuwa yametokea. Akaanza kusema,
"***Mimi ni Yesu, mwokozi wako, kama una mashaka yoyote angalia mikono yangu. Mahali tulikokwenda ni kuzimu***". Nikaona mahali alipogongwa misumari.

Rafiki ningependa nikwambie kuwa kuzimu sio mawazo ya mtu bali ni mahali pabaya pa mateso kulikotengenezewa shetani na mapepo yake. Wanadamu wanastahili kwenda mbinguni pamoja

na Yesu lakini lazima tumchague yeye kabla hatujachelewa. Leo ukisikia sauti yake usiufanye moyo wako kuwa mgumu. Mkubali Yesu kama mwokozi wako, na kama umempokea basi mwishie yeye.

Sikujua sababu ya kuambiwa nichague kati ya makundi mawili huko kuzimu na ilhali mimi nimeokoka. Nimemwamini yeye na bado ananiambia nichague kwenda kuzimu au la. Sikumuelewa. Nikamwomba Mungu anifunulie maana ya usemi huu na kile angetaka nifanye. Akaniambia kuwa nilikuwa mtu wa **HASIRA** na pia **SIKUWASAMEHE** dadangu na binamu yangu mmoja. Nikaomba msamaha kwa dhambi hiyo halafu nikamwomba dada msamaha kwa kuweka hasira na chuki dhidi yake. Ikabakia kwenda kumwomba binamu msamaha.

Bwana akanikumbusha kuwa niliwahi kupata ajira ya ualimu nikitumia cheti bandia cha diploma. Akasema kuwa kitendo hicho ni **DENI** pamoja na **WIZI**. Nilitaka kutenda lililo haki na nikamwomba anipe njia nzuri ya kufuata kwani hilo lilitosha kunipeleka gerezani. Akaniambia nikatubu kwenye idara ya elimu. Nilikuwa tayari kwa lolote, hata kwenda gerezani ikiwa haiwezi kuepukika. Mungu akatenda maajabu na wakuu wakaniambia nichague kama nataka kulipa au la. Hawakutaka kunipeleka mahakamani kwasababu kukiri kwangu kuliwashangaza. Hakika Mungu ni wa ajabu na analiheshimu neno lake.

Ukiwa na jambo kama hili nakusihi kufanya kilicho cha haki bila kujali matokeo. Unaweza ukafungwa jela hapa dunuiani lakini hiyo ni ya muda. Hakuna uchungu au fedheha inayoweza kufananishwa na kutengwa na Mungu milele na milele. Kuzimu sio mahali pazuri; ni afadhali umwache Mungu akuhukumu sasa kabla haujachelewa. Tusiogope hukumu ya Mungu katika siku hizi za neema, NI VYEMA TUMWACHE YEYE ADHIHIRISHE CHOCHOTE KILICHO KIBAYA MAISHANI MWETU KAMA BADO TUNA WAKATI WA KUJIREKEBISHA kwani hakuna msamaha upande ule mwingine wa kaburi.

## SAFARI YA PILI KUZIMU

Tarehe 18/10/2005, niliamka saa kumi na moja unusu alfajiri, sikuweza kwenda kazini. Nilikuwa najisikia dhaifu sana na nikawa nimenyong'onyea; nisingeweza kujisogeza au kugeuka kitandani pangu, uwepo wa Mungu ulikuwa mkubwa chumbani. Nilikuwa nikitetemeka na kuhisi kama nguvu za umeme zinapita mwilini mwangu. Bwana akaja kunichukua kabla ya saa mbili. Alinisalimu na kuniambia kuwa inatupasa kwenda tena kwani **MUDA UMEISHA**. Nikasimama na tukaanza kutembea. Jinsi tulivyokuwa tukitembea siku hii ilikuwa tofauti na siku zingine. Japo miguu yetu ilikuwa ikitembea, ilikuwa ni kama tunaogelea zaidi kuliko kutembea.
Tukiwa safarani, Yesu akaniambia, "***Dhambi zote ni mbaya na hakuna dhambi kubwa wala ndogo. Dhambi zote huleta mauti, haijalishi ukubwa wala udogo***". Akaniambia kuwa tunaelekea tena kuzimu na kisha akaniuliza kama nilikuwa na hofu. Nikamwambia kuwa nilikuwa naogopa. Akasema, "*Roho ya hofu haitoki kwa Baba yangu, inatoka kwa shetani. Hofu itakusababisha ufanye vitu vitakavyo kupeleka kuzimu. Bila imani ni vigumu kumpendeza Mungu na hofu ni kinyume cha imani. Nidhahiri hofu haimpendezi Mungu kwasababu huharibu imani ya mtu ya mtu* ".

Kwa muda wote tukiwa njiani tulikuwa tukitembea upande upande lakini baada ya kufika lango la kuzimu akanishika mkono wangu kwa muda wote tuliokuwa kuzimu. Nilikuwa na furaha kwasababu alinishika mkono na kwa kunishika aliondoa hofu yote ndani yangu. Sehemu hiyo ilikuwa bado inafanana na ya kwanza; hapakuwa na tofauti na sehemu ya kwanza. Kulikuwa na vijidudu virukavyo, minyoo, joto lililokithiri, harufu mbaya, mifupa, kelele. Kila kitu kilikuwa kama nilivyoona mara ya kwanza.

### Mtumishi aishia motoni

Tuliingia lango kama lilelile tena akanipeleka kwenye moja ya makundi ya watu. Kulikuwa na watu wengi niliokuwa nawafahamu walipokuwa hai duniani. Watu walikuwa katika hali mbaya sana; walionekana wamefedheheka na uchungu mzito lakini kibaya zaidi walionyesha sura zisizo na matumaini.

Bwana akamwashiria mwanamke mmoja mwenye umri wa kati. Nilimjua kabla ya kifo chake kilichotokea kwa ajali ya gari mwanzoni mwa 2005. Nilishtushwa kumuona kuzimu kwani sote tulimjua kama mcha Mungu. Bwana akaniambia kuwa mwanamke alimpenda Mungu na Mungu pia alimpenda mwanamke huyo. Alinitumikia alipokuwa duniani, Aliwaongoza wengi kwa Bwana na alimjua Bwana vizuri. Alikuwa mwema kwa maskini na wahitaji; alitoa kwa ajili yao na aliwasaidia katika njia mbali mbali. Alikuwa mtumishi mzuri wa Bwana katika njia nyingi.

Maneno haya ya Bwana yalinishtua sana na zaidi nilipomuuliza kwanini akamwacha mtu aliyemtumikia vizuri aishie kuzimu. Bwana akajibu kuwa ijapokuwa alijua sana maandiko alikubali uongo wa shetani kuwa kuna dhambi ndogo na kubwa. Alifikiri dhambi ndogo haitamwangamiza kuzimu maana yeye ni mkristo. Bwana akaendelea kusema, "***Nilienda mara nyingi na kumwambia aache alichokuwa akikifanya lakini mara nyingi aliendelea kufikiria kuwa dhambi hiyo ni ndogo sana na mwisho akachukulia kuwa maonyo niliyompa yalitokana na dhamiri dhaifu aliyokuwa nayo. Kuna wakati aliacha dhambi hiyo lakini baada ya muda akairudia huku akajishawishi kuwa maonyo hayo ni sauti ya kwake mwenyewe maana dhambi hiyo ni ndogo na haiwezi kumhuzunisha Roho Mtakatifu***".

Nikamuuliza tena Bwana anieleze dhambi aliyoifanya mwanamke huyo, naye akanijibu kwamba, "***Mwanamke huyu alikuwa na rafiki yake Nesi katika hospitali ya Oshakati. Wakati wowote alipokuwa mgonjwa hakuwa akilipia kadi ya hospitali kama inavyotakiwa bali alikuwa anampigia rafiki yake simu na wanafanya mpango wa yeye kupata dawa kutoka kwenye zahanati. Rafiki yake alikubali kumfanyia hivi wakati wote***".

Hukumu yake ni kuwa:

- alikubali uongo wa shetani juu ya dhambi ndogo na kubwa na hivyo kuikataa kweli yangu.
- alimsababisha mwenzie kutenda dhambi ya kuiba kwa niaba yake.
- lililo baya zaidi, alimhuzunisha Roho Mtakatifu. Hii ndio lilimpeleka kuzimu.

"*Haijalishi kama utaleta mamilioni ya nafsi kwa wokovu bado unaweza kuishia kwenda kuzimu kwa kumhuzunisha Roho Mtakatifu. Ni lazima uangalie wokovu wa wenzio lakini uwe mwangalifu usisahau roho yako. Uwe makini na kila jambo unaloambiwa na Roho Mtakatifu*". Baada ya Bwana kuyasema hayo akaniambia turudi.

**<u>Unayachukuliaje maneno haya?</u>**

Wakristo wengi waliosikia simulizi hii hupata maswali mengi. Wanajiuliza,
"Je kuhesabiwa haki, huruma na neema za Mungu hazina nafasi yoyote?".
"Na je unaweza kuupoteza wokovu baada ya kuupokea?".
"Mbona neno hili lina ukali sana? Mungu anaweza kuwa katili hivyo?".

Kama nilivyosema mbeleni mimi sifundishi theolojia. Ninasema tu mambo ambayo Bwna alinionyesha na kunifundisha. Nakuomba uangalie Biblia yako vizuri kwa majibu. Hebu angalia vifungu vifuatavyo halafu ujiamulie.

> *Bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe, nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa. (**1Wakorintho 9:27**)*
>
> *Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi? ( **Warumi 6:1-2**)*
>
> *Basi dhambi isitawale ndani ya mioyo yenu ipatikanayona mauti, hata mkazitii tamaa zake – (**Warumi 6:12**)*
>
> *Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi. Bali kuna kuitazamia hukumu kwenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wao wapingao. (***Waebrania 10:26, 27**)

Je naweza kuishia kwenda kuzimu baada ya kumtumikia Bwana na kuwaongoza wengi kwa Kristo? Jiamulie mwenyewe.

**Kutotii**

Jumatatu tarehe 06/03/2006, niliamka saa kumi na moja na nusu alfajiri. Nilipoanza kuomba nikaona kuna nguvu za Mungu za ajabu juu yangu. Mwili wangu ulikuwa dhaifu na nilikuwa natetemeka. Nguvu kama za umeme zilikuwa zinapita mwilini mwangu.

Mchana nilipokuwa nimelala nikaona mwanga mkubwa wa ajabu ukikijaza chumba chote. Nikaona vitu vidogo vyeupe vyenye umbo la mviringo vikiniangukia kama mvua na kuingia mwilini. Kisha nikaona wingu la kitu kama ukungu likishuka, kukijaza chumba chote na pia kuanza kuingia mwilini mwangu. Nikamwona Yesu akinijia akiwa katikati ya wingu lile la ukungu na akaketia kiti chake kandokando ya kitanda changu. Sijui kiti hicho hutoka wapi ila huwa kinatokea akiwa tayari kukaa. Kiti chenyewe kimeundwa na dhahabu tupu, kuna nyota ya shaba kwenye kila mguu wa kiti hicho. Mahali pa kujiegemezea pamewekwa pia nyota kubwa ya shaba na kila mguu wa kiti hicho kuna magurudumu ya mviringo.

Yesu akaninyoshea mkono kunisalimia. Akaniambia niinuke kwa kuwa **MUDA UMEISHA.** Akanivuta kwa mkono na nikakaa juu ya kitanda. Akaniambia, "***Victoria tuombe***". Akaomba kwa lugha ambayo sikuelewa. Nilichoelewa pekee ni neno 'Amina'. Akaniuliza nilichokuwa naona. Watu walikuwa wakiingia kazini. Nikaona vile vitu vidogo vya mviringo vikiwaangukia kundi la wale waliotangulia kufika mahali pao pa kazi. Waliofika baadaye walipata mvua ya vitu vile imekatika. Jambo hili pia nikaliona kanisani, waliotangulia waliangukiwa na vitu hivi vyeupe lakini waliofika baadaye hawakuvipata.

Yesu akaniuliza kama naelewa maana ya maono hayo nami nikamjibu kuwa, "Sielewi". Basi akanieleza,
*"Maono hayo yana maana kuwa kila mahali unapostahili kufika kwa wakati fulani, na unaujua wakati huo, kuna Malaika wanawagawanya baraka, kwa muda ule. Anayewahi anapata baraka zile anayechelewa anazikosa – kwa kuwa Malaika hugawa baraka kwa muda tu. Vitoria nataka nikuonye kwa kuwa unachelewa kwenda kazini na unachelewa zaidi kwenda kanisani. Elewa kuwa siku ulizochelewa bila sababu umekosa baraka zako za siku hizo milele. Baraka hizo haziwezi kukurudia. Victoria ni lazima uache jambo hilo na usirudie pengine uwe na sababu nzuri".*

Aliponiambia hivyo nilitamani kumkimbia au kumpa sababu nzuri kwa kosa hili. Nikamwambia nilikuwa na tatizo la kulala sana lakini akaniangalia moja kwa moja usoni na kusema kuwa nilikuwa na tatizo la kurudi tena kitandani baada ya kuamka, nilikuwa naangukia majaribu ya kutaka kulala dakika zingine chache.

**Yerusalem Mpya**

Baadaye akaniambia, "***Amka twende MUDA UMEISHA na kuna vitu lazima kuvifanya***". Akanipeleka mahali sijawahi kufika, barabara yenyewe ilikuwa mpya kwangu. Tukafika kwenye bustani yenye maua mazuri na miti mizuri ya kijani kibichi; hakuna kitu duniani cha kulinganisha na uzuri huu. Tukakalia kiti cha dhahabu kilichokuwa kwenye bustani hiyo nzuri.

Tulipokuwa tumekaa, Yesu aliniashiria mbele kwa kidole chake na kusema, "***Victoria angalia, je wauona mji ule***?". Nilipoangalia nikaona mji mkubwa uliokuwa na mwanga mkubwa. Mji huo ulikuwa mzuri kupita maelezo. Lango lake lilikuwa la dhahabu huku liking'aa ajabu, na mtu mwenye umri mkubwa alikuwa amekaa pale. Mtu huyo alikuwa na ndevu na nywele nyeupe. Nilikuwa nimemwona hapo mbeleni na nilipomuuliza Bwana, akaniambia kuwa ni Abrahamu, baba wa Imani.

Niliona barabara nyingi ndani ya mji ule zilizojengwa kwa dhahabu. Kulikuwa na majumba ya ghorofa yalokuwa yaking'aa kama dhahabu. Mng'ao wa jiji lile kwa kweli hauelezeki.
Yesu akanigeukia na kuniuliza, "***Unafikiria nini juu ya mji ule***?"

Nilijibu kuwa ni mji mzuri na nataka niende huko. Yesu akasema, "Nitakupeleka huko ukiendelea kuwa mtiifu, maana ndiko iliko nyumba yako. Ishi kwa uaminifu ukishindwa, nyumba yako

itakaliwa na kunguru na bundi. Itakuwa uwanja wa pepo wabaya. Hata hivyo usihofu, kwasababu niko pamoja nawe, wewe kuwa mtiifu tu. Asiyetii nyumba yake itakuwa makazi ya bundi na uwanja wa mapepo wabaya".

Yesu Kristo kweli yupo na anatupenda kwa upendo usioelezeka. Hitaji kubwa la moyo wake ni wanadamu tuchaguwe uzima ili tukae nae milele.
**Moyo wake unaugua kwa ajili ya watu wanao kufa na kuishia kuzimu** kwasababu ya kuuacha wokovu aliowapa na kuchagua mauti.

Haijalishi umeokoka au haujaokoka neno moja tu ukumbuke ni kuwa: **MUDA KWA HARAKA SANA UNAKWISHA**.